

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA PILI

31 MACHI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA PILI – TAREHE 31 MACHI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**11. MHESHIMIWA HASSAN SELEMANI
MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza ruzuku katika mpango wa utoaji bure Elimu ya Sekondari na Msingi.

**12. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL
ISHENGOMA (VITI MAALUM):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Hospitali ya kisasa Mkoani Morogoro.

13. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaboresha Hospitali ya Wilaya ya Olturumet katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kwa kuipatia Jengo la OPD, Wodi ya kulaza Wagonjwa, Jengo la X-ray na mashine ya X-Ray ili Hospitali hiyo iweze kutoa huduma kwa Wananchi ipasavyo.



WIZARA YA KILIMO:



14. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENAN (NKASI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Utaratibu unaotumika sasa kuwakopesha Matrika Wakulima unawasababishia hasara kwa kuwa wanatozwa riba kubwa:-

Je, kwa nini Serikali isibadili utaratibu huo ili kuleta tija.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

15. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga reli ya TAZARA kutokea Tunduma kwenda Kasanga ili kuwa na manufaa mapana ya kiuchumi na matumizi mazuri ya Bandari ya Kasanga na kuufungua Mkoa wa Rukwa kiuchumi.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

16. MHESHIMIWA ISSA KOMBO OMAR (WINGWI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni kwa nini Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) limewarudisha nyumbani Vijana ambao walishafika Kambini kwa ajili ya kuanza mafunzo.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**17. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani kwa Vijana wanaoshindwa mitihani kwenye ngazi mbalimbali za elimu nchini.

**18. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY
MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni kwa kiwango gani Serikali inajiridhisha kuwa mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya juu imetolewa kwa Wanafunzi walengwa.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**19. MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA
(UKONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na
Mipango:-

Je, Serikali haioni haja ya kurejesha mfumo wa TANEPS Hazina ili utekelezwe na kusimamiwa pamoja na GePG katika kuongeza ufanisi.

20. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itatoa amana na hisa za wateja waliokuwa wamewekeza katika Benki ya Wananchi Meru ambayo ilifungiwa kutoa huduma za kibenki Mwaka 2018.

**DODOMA
31 MACHI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**